# Azimio la Dar es Salaam Juu ya Uhuru wa Uhariri na Uwajibikaji

## Februari 2011

Azimio la Dar es Salaam Juu ya
Uhuru wa Uhariri na Uwajibikaji
Limepitishwa na **Baraza la Habari la Tanzania** na kutangazwa kwa minajili
ya kuridhiwa Dar es Salaam, Machi 18, 2011

**Azimio la Dar es Salaam Juu ya Uhuru wa Uhariri na Uwajibikaji**

Chapa ya Kwanza: Februari 2012
Chapa ya Pili: Januari 2014
Chapa ya Tatu: Julai 2017

© Baraza la Habari Tanzania (MCT), 2012

ISBN 978-9987-710-65-2

# Yaliyomo

**Utangulizi** ........ **v**
Azimio ........ ix
**Sehemu ya I** ........ **1**
Kanuni Elekezi za Msingi ........ 1

**Sehemu ya II** ........ **7**
Majukumu na Wajibu ........ 7
**Sura ya Kwanza** ........ **8**
Dola ........ 8
**Sura ya Pili** ........ **12**
Wamiliki / Wanahisa / Wakurugenzi ........ 12
**Sura ya Tatu** ........ **14**
Watoaji wa matangazo ya kibiashara, Biashara na Wabia wa Kisiasa. 14
**Sura ya Nne** ........ **16**
Wanasiasa / Watendaji wa Serikali ........ 16
**Sura ya Tano** ........ **18**
Wafadhili / Jamii ya Wanadiplomasia ........ 18
**Sura ya Sita** ........ **19**
Maslahi ya Mtazamo Finyu na wa ........ 19
Kishabiki ........ 19
**Sura ya Saba** ........ **20**
Umma ........ 20

**Sehemu ya III** ........ **23**
Kulinda Wanahabari ........ 23

**Sura ya Kwanza ........ 24**
Serikali........ 24
**Sura ya Pili........ 26**
Wahariri Wakuu ........ 26
Sura ya Tatu ........ 27
Wamiliki wa Vyombo vya Habari ........ 27

**Sehemu ya IV ........ 29**
Wajibu wa Wahariri Kijamii ........ 29
**Sura ya Kwanza ........ 30**
Wajibu na Uwajibikaji kwa Umma ........ 30
**Sura ya Pili........ 31**
Rushwa, Uandishi wa Habarikwa........ 31
Kulipwa na Ushawishi ........ 31
**Sura ya Tatu ........ 33**
Vurugu, Chuki na Kukosa Uvumilivu........ 33

**Sehemu ya V ........ 35**
Majukumu ya Wadau Wengine Muhimu. ........ 35

**Sehemu ya VI ........ 37**
Kuidhinishwa na Utekelezaji........ 37
Uhalisia na Uelewa ........ 37
Kuhusu Baraza la Habari Tanzania........ 38
Dhamira........ 38
Dira........ 39

# Utangulizi

Tasnia ya habari nchini Tanzania, kama mahali pengine Afrika, imepitia mabadiliko mengi muhimu. Ingawa kumekuwa na kasi ya ubinafsishaji wa vyombo vya habari, hivyo kufungua fursa mpya za wananchi kupata habari kutoka vyanzo tofauti, dola, imeendelea kujaribu kuzuia uhuru wa uhariri kwa mbinu za waziwazi au kificho na hivyo kudhoofisha upatikanaji wa haki za msingi na uhuru wa habari.

Hata hivyo, mabadiliko katika tasnia ya habari yameibua aina mpya za vitishio katika upatikanaji wa haki za binadamu za msingi, zikiwemo na haki ya kupata habari na kujieleza. Ukiukwaji huu unaendelezwa pia na vyombo vya habari binafsi kutawaliwa na makampuni na mashirika makubwa machache ya habari na kudhibitiwa na watu wachache.

Pamoja na dola na wamiliki binafsi, mashirika yasiyo ya kiserikali yenye ushawishi, nguvu na uwezo wa kuingilia uhuru wa uhariri pia ni tishio

kwa upatikanaji wa haki za msingi na uhuru wa umma.

Haki ya kupata habari na uhuru wa kujieleza ni haki ya mtu binafsi na vilevile haki ya jumla ya jamii. Haki hizi na uhuru zinawekwa wazi na kulindwa na katiba za nchi za Afrika na matamko mbalimbali ya kimataifa na kikanda, ikiwa ni pamoja na Azimio la Kanuni za Uhuru wa Kujieleza Afrika lililopitishwa na Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu la 2002.1

Haki na uhuru wa kupokea, kuchakatua, kusambaza habari, ikiwa ni pamoja na haki na uhuru wa kutoa maoni, ni misingi muhimu ya utawala wa kidemokrasia kisiasa na kiuchumi.

Utekelezaji thabiti wa haki hizi na uhuru huu huwezesha wananchi kushiriki katikautawala wao na hivyo kuthibitisha haki ya watu [1]kujiamulia

1. Katika kikao chake cha kawaida kilichofanyika Banjul Gambia,

tarehe 17-23 Oktoba , 2002

2 . Mkataba wa kimataifa kuhusu Haki za kisiasa na kiraia na mkataba wa kimataifa kuhusu haki sa kijamii, kiuchumi na kiutamaduni.

3. Tamko la umoja wa Mataifa kuhusu haki ya kupata maendeleo, 1986 na Mkataba wa Afrika

4. Azimio la Umoja wa Mataifa kuhusu Mamlaka juu ya Mali Asili, 1962

mambo yao wenyewe, jambo ambalo limetambuliwa na kutetetwa sana na mikatabayote ya kimataifa na kikanda,ukiwemo Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu,1982 na Azimio la Ulimwengu la Haki za Binadamu 1948.Kwa Afrika ya leo, haki ya watu kuamua mambo yao wenyewe kisiasa na kiuchumi 2 ni muhimu kwaupatikanaji wa haki ya kupata maendeleo 3 na utetezi wa mamlaka yao ya kudumu juu ya mali asili zao.4

Wazingatiaji wa haki hizi za msingi ni wananchi wenyewe, kwa pamoja na mmoja mmoja. Walioweka sahihi katika Azimio hili la Uhuru wa Uhariri na Uwajibikaji wanaelewa fika kuwa upatikanaji wa haki hizi unahitaji vyombo vya habari vilivyo huru, kuhusu Haki za Binadamu na watu, 1982 makini na hai na vinavyoendeshwa na kuongozwa na watendaji wenye maadili mema.

Uhuru wa vyombo vya habari ni lazima uambatane na uhuru wa wana habari katika kutekeleza majukumu yao bila woga wala upendeleo na hasa, bila kuogopa shinikizo za kisiasa, kiuchumi na maslahi mengine binafsi ndani ya jamii.Vyanzo vya shinikizo kwa vyombo vya habari vinatofautiana lakini muhimu kati yao, ni dola na wafanyabishara

binafsi ambao wanadhibiti siasa na uchumi wa taifa.

Wamiliki binafsi wa vyombo vya habari wanapaswa kutambua kuwa umiliki wao si wa kipekeeau kwa ajili ya watu maalum tu. Tasnia ya habari ni mali ya umma na inahudumia maslahi ya umma. Kwa hivyo basi, upatikanaji wa faida, jambo linalosukuma umiliki binafsi, unahitaji kupewa kipaumbele cha chini kulinganisha na maslahi halali ya umma, ambayo ni kuhakikisha utekelezaji wa haki za msingi na uhuru uliojadiliwa awali. Hii ina maana kuwa maslahi ya umma na uwajibikaji kwa umma vina umuhimu kuzidi haki na maslahi ya umiliki binafsi; kwa mantiki ya kuwa, vyombo binafsi vipo kwa ajili ya maslahi ya umma na vinatoa huduma kwa umma na kwamba, wamiliki na watendaji wanawajibika kwa umma.

Kwa kuzingatia masuala haya, mwaka 2006, Baraza la Habari Tanzania (MCT) lilianzisha mchakato wa kuandaa sheria mbili muhimu kuhusu Haki ya Kupata Habari na Huduma za Vyombo vya Habari. Baada ya mashauriano yaliyohusisha wadau kutoka sehemu zote za nchi na yaliyodumu kwa kipindi cha miaka miwili, rasimu mbili zilizotayarishwa na washiriki kutoka mashirika yasiyo ya kiserkali, wana

habari, na washiriki wengine wa taasisi za kiraia, ziliwasilishwa kwa Serikali ya Tanzania.

Aidha, kwa kutambua umuhimu wa uhuru wa uhariri, kuanzia mwaka 2008, MCT ilianzisha na kuwezesha mchakato wa kutayarisha Azimio hili.

Azimio hili limebuniwa katika misingi kuwa ni mali ya jamii ya wadau ambao wanabeba jukumu la kutelekeza yaliyomo ndani yake.

Azimio hili sasa liko tayari kwa kuidhinishwa na kuwekwa sahihi.

## Azimio

Kwa kutambua umuhimu wa uhuru wa uhariri na uwajibikaji kijamii katika kujenga vyombo vya habari vyenye nguvu na huru;

Kwa kuelewa majukumu makubwa kijamii na kisiasa ya vyombo vya habari huru katika upatikanaji wa haki za watu, kwa pamoja, kujiamulia mambo yao wenyewe kisiasa na kiuchumi, haki za msingi za mtu binafsi kama zinavyotambuliwa na kanuni mbalimbali kimataifa na kikanda , pamoja na katiba za nchi;

Kwa kutambua umuhimu wa haki ya watu wa

Afrika kutetea umiliki wao wa kudumu wa mali asili kwa maslahi ya maendeleo endelevu ya nchi zao na; Kwa kufahamu nafasi ya vyombo vya habari katika kupambana na uwakilishi hasi wa wanawake na wanaume na mitazamo hasi kijinsia katika jamii;

Kutokana na wasiwasi juu ya kuongezeka kwa kasi ya uporaji wa kudhamiria na utekaji nyara wa maliasili na mali nyingine nchini Tanzania na katika bara lote la Afrika katika miongo mitatu iliyopita;

Kwa kuamini kuwa mtiririko huru wa habari, majadiliano na utoaji maoni ni kichocheo muhimu katika kuhamasisha jamii na kuongeza uelewa wa watu katika kupigania haki na uhuru wao nakutetea mamlaka yao kisiasa na kiuchumi;

Kwa kufahamu kuwa vyombo vya habari vya kielektroniki vinaruhusu upatikanaji wa habari usio na mipaka kwa kila mtu, pamoja na watoto na wengine wasiokuwa na uwezo wa kuchuja na kutathmini usahihi wa maudhui yanayowasilishwa;

*Kwa hiyo sasa wawekaji sahihi katika Azimio hili wanadhamiria:*

1. Kutangaza, kushawishi na kuendesha kampeni ya kuungwa mkono kwa wingi kwa Azimio

hili na watendaji na wadau wote, pamoja na watendaji wa ndani na nje ya dola ndani ya nchi na katika ukanda wa Africa;

2. Kujitahidi kuzingatia misingi ya Azimio hili na kutayarisha mifumo rasmi na isiyo rasmi ya utekelezaji;

3. Kushawishi mashirika ya kitaaluma, utafiti na kitaalam, umuhimu wa kujumuisha Azimio hili na kanuni zake za msingi katika mipango yao ya mafunzo na utafiti.

4. Kudai kuwa majukumu yanayohitaji kutambuliwa rasmi yaingizwe katika hati maalum na makubaliano kati ya umma na wamiliki wa vyombo vya habari binafsi kwa upande mmoja na watendaji kwa upande mwingine;

5. Kudai kuwa watendaji wasiokuwa wa serikali, mbali na wamiliki, watambue na kuunga mkono hadharani Azimio hili pamoja na misingi yake muhimu na kuizingatia katika mahusiano yao na vyombo vya habari; na

6. Kudai kuwa watendaji wote wenye madaraka

waache tabia ya kuingilia uhuru wa uhariri. Aidha, wawekaji sahihi wa Azimio hili wanatoa wito kwa wana habari wote kwa ujumla na hasa kwa wahariri;

7. Kupinga ushawishi, shinikizo na motisha kutoka kwa washiriki kutoka nje zinazoweza kudhoofishauhuru wa uhariri na kuingilia maamuzi yao kwa kuzingatia viwango vya kitaalamu na kanuni za msingi za Azimio hili;

8. Kutekeleza wajibu wao na majukumu yao kijamii kwa uadilifu mkubwa, umakini na umahiri unaolingana na viwango vya kitaalamu na maadili; na

9. Kuelewa wakati wote kuwa wajibu na uwajibikaji wao ni kwa umma na kuwa wao ni watendaji wa umma wanaotoa huduma katika nyanja nyeti ya utumishi kwa umma kwa minajili ya kujenga jamii ya kidemokrasia, isiyo na ukandamizaji; isiyo na ubaguzi kwa misingi ya rangi,ukabila, jinsia na ulemavu; na isiyo na uvunjaji wa haki za binadamu.

# Sehemu ya I

## Kanuni Elekezi za Msingi

Kanuni za msingi zilizoelezwa hapo chini ni sehemu muhimu ya Azimio hili. Kanuni hizi zitatoa mwongozo kwa tafsiri na utekelezaji na zitazingatiwa katika kuingia mikataba kati ya wamiliki na watendaji na katika kutunga sera za uhariri na makala mengine ya kisera.

1. Uhuru wa kujieleza, ambao ni pamoja nahaki ya msingi ya kupokea, kuchakata na kusambaza habari, ni haki ya umma kwa pamoja na mtu mmoja mmoja.
2. Wajibu wa msingi wa wamiliki wa vyombo vya habari na watendaji ni kuwezesha umma, kwa pamoja au kwa mtu mmoja mmoja, kupata na kufaidi haki na uhuru wa habari.

3. Wamiliki wa vyombo vya habari na wana habari wanawajibika kwa umma.
4. Wanahabari wote wanapaswa kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia ukweli, uadilifu, umahiri na weledi pamoja na umakini na uwajibikaji wa hali ya juu kwa umma, ili kujenga imani na uaminifu machoni kwa umma.
5. Wanahabari wanapaswa kujenga umoja wa kijamii, kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni kwa kukuza uvumilivu wa tofauti za maoni na imani.
6. Wamiliki wa vyombo vya habari na waandishi wa habari lazima wachukue hatua za kulinda haki za mtoto na heshima ya watoto kwa kuongeza uelewa wa umma katika masuala kama vile vurugu zinazotokana na mitandao, biashara ya kuuza watoto na utumwa wa ngono.
7. Wamiliki wa vyombo vya habari na wanahabari wanawajibika kuendeleza na kuwezesha mazungumzo na mijadala ya umma na usambazaji wa mawazo na habari.

Kwa hiyo basi, wanapaswa kutoa fursa za mazungumzo na mijadala hiyo katika vyombo vyao vya habari.

8. Wanahabari wanawajibika kukuza heshima ya binadamu, kupambana na aina zote za ubaguzi na kukuza usawa kati ya wanawake na wanaume katika jamii nawakati huo huo kupambana na ubaguzi wa kila aina.

9. Wanahabari wanawajibika kuepuka tabia ya kuchochea au kusababisha uchochezi wa vurugu, chuki na ubaguzi dhidi ya wageni na daima kuzingatia ukweli wa hali ya juu. Ni wajibu, hasa wa wahariri, kutoa maamuzi yenye hekima na busarakatika kuchapisha habari na maoni yanayoweza kuchochea vurugu, chuki na ubaguzi dhidi ya wageni.

10. Watendaji wote waliotajwa katika sehemu ya 1 ya Azimio hili wanawajibika kujizuia kuingilia wahariri na wanahabari kwa namna inayoweza kudhoofisha uhuru wa uhariri.

11. Ni haki ya msingi kwa wananchi kupata habari bila kizuizi. Serikali, wamiliki wa vyombo

vya habari na wanahabari wanapaswa kuwezesha upatikanaji wa habari huo na daima kukumbuka kuwa fursa na haki ya kupata habari ni kwa manufaa ya umma.

12. Wamiliki wa vyombo vya habari na wanahabari wanawajibika kubuni njia, kama vile kamati za kuchunga vyombo vya habari, zinazojumuisha wajumbe kutoka asasi za kiraia wenye uadilifu wa hali ya juu, kuwezesha kushiriki kwa umma katika kusimamia vyombo vya habari nakuhakikisha vinatimiza wajibu wao kwa maslahi ya umma.

13. Ili kuhakikisha kuwepo kwa uanuai na urahisi wa upatikanaji wa habari za ukweli na makini, wanahabari nawahusika wengine wote wa vyombo vya habari wanapaswa kujitahidi kuzuia ukiritimba, pamoja na kutoruhusu watu wachache kuhodhi vyanzo vya habari na kupinga bila kuchoka muungano na urithishaji wa umiliki utakaopelekea ukiritimba na kuhodhi kwa namna hii.

14. Wadau wa vyombo vya habari wanapaswa

kuhimiza umiliki na utawala wenye mfumo wa ushirika na unaoendeshwa na wanahabari wenyewe.

15. Wahusika wote lazima washirikiane kugeuza vyombo vya habari vinavyomilikiwa na serikali kuwa vya umma, vinavyowajibika kwa umma kupitia vyombo vya uwakilishi kama vile Bunge.

16. Wanahabari walio katika nafasi za kutoa maamuzi, wanawajibika kuwekaurari kati ya matangazo ya kulipiwa na habari.

# Sehemu ya II

## Majukumu na Wajibu

Watendaji wote wakuu wa vyombo vya habari wanabeba jukumu na wajibu wa kukuza na kulinda uhuru wa uhariri ili kuhakikisha kuwa wahariri na wanahabari wengine wana uhuru wa kufanya maamuzi yanayozingatia matakwa ya kitaalam na masharti ya kimaadili.

## Dola

Pamoja na kasi ya ubinafsishaji wa vyombo vya habari, Serikali bado ina majukumu muhimu kisheria na kiutawala ambayo wakati mwingine huingilia uhuru wa kujieleza na uhuru wa uhariri. Kwa hivyo basi, Serikali ina wajibu na majukumu kadhaa katika kuhakikisha kuwepo mazingira bora ya vyombo vya habari.

17. Hatua zinapaswa kuchukuliwa kugeuza vyombo vya habari vya serikali kuwa vya umma , vinavyoanzishwa kwa mujibu wa sheria inayopitishwa na Bunge na kufadhiliwa kupitia bajeti ya Bunge.

    Uteuzi wa wahariri na watendaji wengine kuendesha vyombo hivi, pamoja na kutoa mwelekeo wa kisera, uwekwe mikononi mwa vyombovisivyofungamana na upande fulani navinavyowakilisha matakwa ya umma, pamoja na kuwa namamlaka ya kuwahudumia

wananchi wote bila upendeleo au kizuizi.

18. Serikali isitumie sheria kuzuia au kubana uhuru wa uhariri kwa kupitia sheria za kibabe kama zile zinazofanya kashfa kuwa kosa la jinai. Sheria zinazohusu kulinda hadhi za watu zinapaswa kuwa katika nyanja ya sheria ya madai.

19. Kanuni za Usajili na utoaji leseni zisiathiri uhuru wa uhariri. Pasiwepo na sheria zinazompa waziri au afisa wa serikali madaraka yasiyokuwa na mipaka, kupiga marufuku, kukataza, kusimamisha au kubana vyombo vya habari, kwa vile madaraka kama hayo, mara nyingi, hutumiwa kuingilia au kutoa vitisho kwa uhuru wa uhariri.

20. Mipaka yeyote kwa uhuru wa uhariri, kwa misingi ya kuzingatia usalama wa taifa, ni lazima katika jamii yeyote ya kidemokrasia na hutumika kwa madhumuni halali. Mipaka hiyo, hata hivyo, lazima itumike kwa busara na lazima itolewe ufafanuzi wa wazi na ufasaha na izingatiwe kwa makini.

21. Katika kesi zinazohusu kashfa na madai mengine yanayofanana nayo, mahakama lazima yatambue umuhimu wa kukuza uhuru wa uhariri ili kupanua wigo wa haki za msingi za umma. Mahakama yazuie ulipishaji wa fidia kubwa kupita kiasi kwa kesi za kashfa ambazo matokeo yake ni kufilisi vyombo vya habari na kwa hivyo kujenga tabia ya kuvifanya vyombo vya habari kujidhibiti vyenyewe na kukatisha tamaa uandishi wa habari unaotumia uchunguzi wa kina.

22. Mahakama yanapaswa kutenganisha kesi za kashfa zinazohusu watumishi wa umma na watu binafsi. Kwa kukubali nyadhifa na uongozi wa umma wahusika hawanabudi kukubali kukosolewa na kuhakikiwa na umma. Mahakama yanapaswa kuwezesha hatua hii muhimu kwa kutoa tafsiri zenye kubana maana ya kashfa katika kesi zinazohusika na viongozi wa umma.

23. Serikali inapaswa kuondokana na tabia ya kutumia ubabe unaozuia uhuru wa uhariri, kama vile vitisho vya polisi, kufungwa jela

kwa waandishi wa habari, kunyang'anya na kuharibu vitendea kazi vya habari. Pale ambapo mawakala wa serikali watapatikana na shutuma za kutenda ukatili dhidi ya wanahabari, uchunguzi makini lazima ufanyike na wahusika washughulikiwe kwa uthabiti na uwazi.

24. Serikali isitumie uwezo wake wa kuwa chanzo kikuu cha habari na mapato yatokanayo na matangazo ya kibiashara kukataa kutoa habari au matangazo ya kibiashara kwa vyombo vya habari inavyoona kuwa si rafiki. Matangazo ya kibiashara lazima yatolewe kutumia vigezo halali kama vile uwezo wa kufikia na kushawishi watu wengi.

25. Serikali inapaswa kuchukua hatua za kuzuiauchapishaji wa matangazo ya kibiashara yanayoendeleza taswira hasi za wanawake na wanaume katika jamii.

## Wamiliki / Wanahisa / Wakurugenzi

Miundo ya umiliki wa vyombo vingi vya habari inajumuisha matabaka ya watu ambao, kwa kutumia ushawishi unaotokana na wao kuwa wamiliki, wanahisa au wakurugenzi; wanaweza kuwa chanzo cha kuingilia kwa kiwango cha kutisha , na kumomonyoka kwa uhuru wa uhariri. Ni muhimu kwa watu hawa na maslahi wanayowakilisha, kujizuia kutumia ushawishi wao kwa namna ambayo haiendani na uhuru wa uhariri.

26. Wamiliki wa vyombo vya habari wasitumie uwezo wao wa kufanya maamuzi ambao unaathiri kazi za wahariri na wana habari wengine katika masuala kama vile uajiri, mafunzo, maendeleo na usalama kazini, kutoa upendeleo au motisha kuzuia uhuru wa wanahabari. Uteuzi wa wahariri na waandishi wa habari,pamoja na mafunzo, kupanda cheo na maslahi, lazima uzingatie sifa na uwezo,

bila kuingiliwa na masuala mengine, kama vile uhusiano wa kifamilia.

27. Wahariri lazima wafaidike na mikataba inayowapa usalama wa ajira na kufukuzwa kwao kazini kutokane tu na utovu wa nidhamu au uzembe na baada ya uchunguzi kikamilifu kukamilika.

28. Mazingira ya uhaba mkubwa wa ajira usitumike kuleta shinikizo zinazokiuka maadili kwa wahariri na waandishi wa habari au kusababisha madai yasiyo halali kwao au ushawishi utakaopelekea utendaji unaokwenda kinyume na kanuni za kitaalamu.

29. Umiliki mseto wa vyombo vya habari na aina nyingine za umiliki na uendeshaji, kama vile ushirika wa wanahabari, unahitaji kuhimizwa na wadau wote ili kuwezesha umma kupata vyanzo tofauti vya taarifa, habari na maoni.

30. Wamiliki wa vyombo vya habari wanapaswa kuweka sera zinazohusu unyanyasaji wa kijinsia ili kuwalinda wanawake na wanaume kutokana na unyanyasaji huo.

# Sura ya Tatu

## Watoaji wa matangazo ya kibiashara, Biashara na Wabia wa Kisiasa.

Upo uhusiano kati ya wafanya biashara, wabia wa kisiasa wa wamiliki na wanahabari, wakishindania matangazo ya biashara ambayo ndiyo uti wa mgongo wa mapato ya vyombo vya habari. Kulingana na haliilivyo katika tasnia ya habari, jambo hili linaweza kuathiri vibaya uhuru wa uhariri.

31. Mashirika ya kibiashara , ambayo ni chanzo kikuu cha pili cha mapato yatokanayo na matangazo, baada ya serikali, yasitumie nguvu hii kuadhibu au kushinikiza vyombo vya habari vinavyochapisha au kuonekana kuchapisha habari zisizoendana na maslahi yao. wa vyombo vya habari wasisalimu amri kwa shinikizo kutoka kwa wafanyabiashara wasiokuwa waaminifu kwa hofu ya kupoteza mapato yatokanayo na matangazo. Kwa

vyovyote vile wamiliki wasiwakandamize wahariri wao na watendaji wengine kwa kutupilia mbali makala yenye maslahi kwa umma kwa kuhofia kupoteza mapato yatokanayo na matangazo.

32. Wanahabari lazima wajitahidi kulinda heshima ya wanawake kwa kukataa kuchapisha matangazo ya unyanyasaji wa kijinsia.

33. Wamiliki wa vyombo vya habari wasitumie mahusiano yao na wanasiasa au wafanya biashara wakubwa kubadilisha makala au tahariri.Wahariri wanapaswa kutoruhusu mahusiano ya kisiasa na kibiashara ya wamiliki wao kuathiri makala yao au kwa kwa njia yeyote ile kuingilia busara za maamuzi yao kiuhariri.

## Wanasiasa / Watendaji wa Serikali

Wanasiasa na watendaji wa Serkali siku zote wana shauku kubwa na mwenendo wa vyombo vya habari na hutafuta kuvishawishi kutoa habari zinazokidhi maslahi yao. Wahariri wanapaswa kuchunga sana ushawishi huu na kuepukana na kukuza mahusiano yanoyoweza kudhoofisha ufanisi wao.

34. Pamoja na kuwa ni muhimu kuwa na mawasiliano na wanasiasa na asasi za kisiasa, wahariri na wanahabari wengine lazima kujilinda na kujenga uhusiano wa karibu mno na wanasiasa au kujiingiza ndani ya mifumo ya kisiasa, mambo ambayoyanaweza kuifanya kazi yao kuwa ngumu na kusababisha ukosefu wa umahiri katika uanahabari. Uhusiano wowoteunaopelekea mgongano wa maslahi, lazima uwekwe bayana kwa msomaji au mtazamaji ili kuhakikisha uwazi.

35. Wanasiasa, ikiwa ni pamoja na wale ambao ni wamiliki wa vyombo vya habari, lazima waache kutumia vyombo vya habari na wafanyakazi wao kwa ajili ya kuendeleza maslahi yao finyu ya kisiasa, dhidi ya majukumu ya vyombo vya habari kuwakilisha maslahi ya umma.

# Sura ya Tano

## Wafadhili / Jamii ya Wanadiplomasia

Baadhi ya wafadhili na jamii ya wanadiplomasia hudai kuwa na nia ya kukuza uhuru zaidi wa habari, ikiwa ni pamoja na uhuru wa uhariri.

36. Wafadhili na jamii ya wanadiplomasia wanapaswa kuepuka kunyakua haki za raia kufanya maamuzi yao wenyewe kuhusu uhuru wa habari. Wanapaswa kuacha kutumia uwezo wao wa kifedha kutanguliza ajenda za mataifa yao na kuweka kando agenda za kitaifa.

37. Msaada wa wafadhili na fedha zitolewe kwa misingi ya msaada wa awali wenye nia ya kuchagiza juhudi za wananchi kupata uwezo wa kujitegemea wenyewe.

## Maslahi ya Mtazamo Finyu na wa Kishabiki

38. Wahariri lazima daima kupinga shinikizo kutoka kwa makundi yanayowasilisha maslahi finyu na ya kiushabiki na kuepuka kuyapa umaarufu wasiostahili au kutetea malengo maalum.

39. Wahariri na waandishi wa habari lazima daima kukataa madai yasiyokuwa na mantiki na yanayokiuka maadili kutoka kwa makundi yao ya kijamii kama haya yanaweza kuwafanya kuwa na mitazamo finyu na kuwasababisha kufikiri kimakundi na kujifunga kimawazo.

# Sura ya Saba

## Umma

Kutokana na kwamba jukumu la vyombo vya habari ni kuutumikia umma kwa kutoa fursa kwa ajili ya kubadilishana habari na maoni, umma kwa upande wake una wajibu wa kuwa macho na kudai viwango vya juu kabisa vya weledi kutoka kwa vyombo vya habari kwa kushiriki katika utoaji na upatikanaji wa habari:

40. Umma, lazima ukuze na kulinda uhuru wa habari kama sehemu muhimu ya masuala mapana ya utawala wa kidemokrasia na maendeleo.

41. Umma, lazima uviwajibishe vyombo vya habari kwa kuandika barua kwa wahariri na kutoa mirejesho mingine kusahihisha makosa na kujadiliana na waandishi wa habari kuhusu uwasilishaji wao wa masuala mbalimbali.

42. Umma una haki na wajibu wa kushiriki vizuri katika utoaji wa habari , taarifa na maoni na

pia kuchukua fursa ya aina mpya za mitandao vyombo vya habari kukuza uandishi wa habari wa raia.

# Sehemu ya III

## Kulinda Wanahabari

Vyombo vya habari huru na vinavyojitegemea vinategemea kuwepo kwa kundi la wataalam wanaoweza kutekeleza majukumu yao bila kuingiliwa ovyo, kupata shinikizo au vitisho kutoka kwa wenye nguvu. Hawa ni pamoja na serikali, wamiliki wa vyombo vya habari, wanasiasa na makundi yawafanyabiashara katika jamii. Ushindani wa wakati huu, ndani na nje ya vyombo vya habari, umewaletea wanahabari aina mpya za vitisho na hatari. Kwa hiyo ni lazima hatua zichukuliwe kuwalinda wanahabari katika kutekeleza majukumu yao. Uhuru wa kuondokana na vitisho utaimarisha uhuru wa uhariri na kukuza vyombo vya habari vyenye kujiwekea viwango vya juu vya weledi na maadili.

## Serikali

43. Wanahabari wote wana haki ya kutimiza majukumu yao ya kuchunguza, kupiga picha, kupiga picha za filamu, kuandika na kutoa habari na huduma bila hofu ya kuingiliwa , kunyanyaswa, kutishwa, kuzuiwa, au kukandamizwa na serikali au mamlaka yeyote ya umma.

44. Wanahabari wote wanahitaji kutumia vyanzo vyao vya habari vya siri bila hofu ya kulazimishwa kuvitaja, isipokuwa kwa amri halali ya mahakama au pale ambapo maslahi ya umma yanazidi umuhimu wa usiri. Wahariri wakuu watachukua vyanzo vya habari kutoka kwa waandishi wa habari na kuvilinda.

45. Pale ambapo upande wowote unadai kupewa chanzo cha habari, itakuwa ni juu yake kuthibitisha umuhimu na ulazima wa kupewa

chanzo cha habari.

46. Mamlaka ya mahakama yanapaswa kuweka mipaka kwa tafsiri ya sheria za uchapishaji wa habari zinazohusu usalama wa taifa na siri za serikali, ili mradi sheria zenyewe ni nzuri , za lazima na muhimu katika jamii ya kidemokrasia, ili umma usinyimwe habari muhimu bila sababu za kutosha.

47. Vyombo vya kiserikali vina wajibu kulinda waandishi wa habari ambao wanaweza kuwa katika hatari ya kudhurika binafsi au ofisi zao au vitendea kazi vyao hadi hatari hiyo ipite.

## Wahariri Wakuu

48. Wahariri wakuu wana wajibu wa kulinda na kuwakinga waandishi wa habari kutokana na kuingiliwa,unyanyasaji, vitisho, au ukandamizaji wanaoweza kukumbana nao kutoka kwa serikali, asasi za kisiasa, makundi ya kibiashara, waajiri na wamiliki.

49. Wahariri wakuu wanapaswa kuhakikisha kuwa waandishi wa habari wanalindwa kutokana na ushawishi wa nje na vishawishi kutoka vyanzo vingine kwa kuwapatia malipo ya haki na mazingira mazuri ya kazi.

50. Wahariri wakuu wanao wajibu kudumisha viwango vya taaluma na uadilifu miongoni mwa wafanyakazi wao kwa njia ya uajiri unaozingatia sifa, taratibu, fursa za mafunzo, ukaguzi wa kazi wa mara kwa mara na kupanua uzoefu wa kazi.

# Sura ya Tatu

## Wamiliki wa Vyombo vya Habari

51. Wamiliki wa vyombo vya habari wanahimizwa kuweka, kwa kushauriana na wahariri wao wakuu, kamati za ndani zenye uhuru wa kupokea malalamiko kutoka kwa wafanyakazi.

52. Wanahabari wanapaswa kujisikia huru kutoingiliwa katika utekelezaji wa majukumu yao kwa kuingia mikataba na wamiliki wa vyombo vya habari ambayo itawahakikishia uhuru wa uhariri na kupunguza ushawishi unaotokana na maslahi ya kisiasa na kibiashara.

# Sehemu ya IV

## Wajibu wa Wahariri Kijamii

Wahariri, kwa mujibu wa kazi yao, wanapaswa kubeba majukumu makubwa kama waamuzi wa mwisho wa jambo gani lichapishwe na kwa hiyo wanatakiwa kuwa na msimamo, kuzingatia haki na uadilifu.

## Wajibu na Uwajibikaji kwa Umma

53. Uhuru wa uhariri lazima uwe na maana ya uhuru wa umma kupata habariambazo zimechakatwa na kusambazwa na wahariri na waandishi wa habari wengine.

54. Wahariri wanapaswa kuchukuatahadhari kubwa kutofautisha tahariri, makala na matangazo ya kibiashara,na makala zilizolipiwa ili kuudanganya au kuuchanganya umma kuhusu chanzo na asili ya maudhui.

55. Wahariri wanapaswa kuwa waangalifu wanapotumia vyanzo kama vile matangazo rasmi au maelezo yanayotokana na idara za serikali, mashirika ya kibiashara, balozi na mashirika mengine rasmi kwa kuyapima kwa umakini na kuchunguza uhalisia wake.

## Rushwa, Uandishi wa Habarikwa Kulipwa na Ushawishi

56. Wahariri lazima wajitahidi kuwajengea wanahabari wao amali za uaminifu, uadilifu, na kujitoa kuhudumia umma; waandishi wa habari wanapaswa kutokuomba au kutokupokea aina yeyote ya motisha isiyo halali.

57. Uandishi wa habari kwa kulipwa lazima upigwe vita na waandishi wa habari wanahitaji kulelewa katika mazingira yanayochukia rushwa kama adui wa kwanza anayehitaji kupigwa vita na wote.

58. Wahariri wana wajibu wa kutoa mafunzo kwa waandishi wao wa habari kutambua aina mbalimbali ya vishawishi vinavyoweza kuwashushia hadhi wao na kazi zao, ikiwa ni pamoja na fedha na zawadi nyingine kama vile

chakula, vinywaji na usafiri wawepo kazini.

59. Wahariri wanatakiwa kuchunguzamadai yote na matendo yote yanayoashiria rushwa na kuchukua hatua madhubuti dhidi ya madai yote yatakayothibitishwa kuwa ni kweli ili kumaliza rushwa ndani ya vyumba vya habari. Kwa vyovyote vile, mwandishi wa habari aliyehusishwa na rushwa asiruhusiwe kuendelea kufanya kazi katika vyumba vya habari.

## Vurugu, Chuki na Kukosa Uvumilivu

60. Wahariri lazima kuepuka kuzipa umuhimu usiostahili makala na taharirri zinaendeleza vurugu, chuki, na ubaguzi kwa misingi ya dini, rangi, na ukabila, ambavyo vinaweza kusababisha kutokuelewana au kujenga ubaguzi wa kijinsia na aina nyingine za ubaguzi kijamii.

61. Ulinzi wa vikundi vya watu walio katika mazingira magumu,kama vile watoto, walemavu na waathirika wa unyanyasaji, ni jambo muhimu sana.Mahsusi, habari zenye vielelezo kuhusu unyanyasaji wa kijinsia lazima zitumike kuhamasisha kuwepo kwa sera za kukataa kabisa kuwepo kwa unyanyasaji wa kijinsia. Kwa hiyo wahariri wana wajibu kuongoza waandishi wao wa habari kuhusu njia muafaka za kupata makala kuhusu makundi na masuala haya.

62. Katika mijadala na mazungumzo yoyote ya umma,wahariri wanapaswa kuzipa pande zote za mjadala nafasi na uzito sawa na kuhakikisha kuwa kila aina ya maoni ya umma imesikika na kuwa misimamo yote muhimu imeelezwa kwa usawa na haki.

# Sehemu ya V

## Majukumu ya Wadau Wengine Muhimu.

Ulinzi wa uhuru wa uhariri ni mapambano ya kudumu yanayohitaji kuungwa mkono na wadau nje ya asasi za habari ili kusonga mbele.Uwezo wa vyombo vya habari katika nyanja za utafiti, mafunzo, uhamasishaji, na kuamsha mwamko mara nyingi ni mdogo au haupo kabisa, na kwa hiyo basi vinahitaji kusaidiwa na asasi nyingine zenye uwezo huo.

63. Taasisi za kitaaluma, utafiti na asasi za kitaalam ambazo hutoa mafunzokwa waandishi wa habari zina wajibu wa kuingiza uhuru wa uhariri katika mitaala yao.

64. Asasi za kiraia na makundi mengine ya uhamasishaji yana wajibu wa kushawishi na

kutetea uhuru wa uhariri na uwajibikaji kwa nia ya kujenga jamii ya kidemokrasia.

65. Vyama vya kitaalam venye ushawishi mkubwa lazima visaidie kuimarisha weledi katika tasnia ya habari kwa kuendeleza mipango ya elimu na majadiliano ya mara kwa mara na umma kuhusu masuala ya uhuru wa kujieleza, uhuru wa uhariri na masuala mengine ya wakati huu katika nyanja ya mawasiliano na umma.

66. Mashirika ya vyombo vya habari yanapaswa kuanzisha utaratibu wa kisayansi wa kupimana kati ya taasisi zinazofanana na kufanya ukaguzi wa mara kwa mara katika nyanja za uhuru wa uhariri, weledi, na uadilifu katika uandishi, ambao unaweza kutangazwa kwa umma.

# Sehemu ya VI

## Kuidhinishwa na Utekelezaji

67. Wadau wanaweza kukubaliana na Azimio hili kwa kuweka sahihi nakala yake kwa niaba ya mashirika yao au kwa niaba yao binafsi kama wananchi na kuiwasilisha nakala hiyo kwaBaraza la Habari Tanzania.

68. Kwa kusaini Azimio hili, mwekaji sahihi anakubali kufanya yafuatayo;

- Kufuata kanuni zake za msingi
- Kutangaza, kueneza na kulipigia kampeni kwa namna zinazofaa na zinazoendana na mazingira husika.

### Uhalisia na Uelewa

Makala ya Kiswahili na Kiingereza ya Azimio hili yatachukuliwa kuwa tafsiri sahihi na utekelezaji

wake utaongozwa na yale yaliyomo katika sehemu ya Utangulizi na ileya Kanuni Elekezi za Msingi, ambazo ni sehemu muhimu za Azimio hili.

Limeidhinishwa na Baraza la Habari Tanzania na kuruhusiwa kusainiwa Dar es Salaam siku hii

ya 18th ....................siku hii ya February ..............................2011

**Mhe, Jaji Dkt. Robert H. Kisanga**
**Raisi**

..................................................................

**Kajubi D. Mukajanga**
**Katibu Mtendaji**

..................................................................

## Kuhusu Baraza la Habari Tanzania

Baraza la Habari Tanzania (MCT) liliundwa Juni 30, 1995. MCT ni chombo huru, kisicho cha kiserikali ambacho lengo lake kuu ni kusaidia kukuza na kuimarisha uhuru wa vyombo vya habari Tanzania.

## Dhamira

Dhamira ya MCT ni kuweka mazingira mazuri ambayo yatawezesha kukua na kuimarika kwa tasnia ya habari inayozingatia maadili ya kitaaluma ambayo yatachangia kikamilifu katika kujenga jamii inayozingatia demokrasia na haki.

## Dira

Kuwa na Tanzania iliyojengeka katika misingi thabiti ya demokrasia ambayo ina vyombo vya habari huru, vinavyoheshimika na vyenye kuchangia mustakabali wa maendeleo ya nchi.